Mreno kaua watu 3

Mwafrica 13-9-63

WATU watatu wameuliwa na askari wa Kireno huko Msumbiji baada ya watu hao kugunduliwa kwamba ni wanachama wa FRELIMO. Mmoja miongoni mwa watu hao alikuwa ni mwanamke'

Habari hizi zimetangazwa leo mjini Dar es Salaam na Katibu wa Habari katika ofisi Kuu ya FRELIMO, Bw. Chiteji.

Alisema kwamba mtu wa kwanza ambaye jina lake halijulikani ni wa kijiji cha Kunuma. Yeye baada ya habari kufikishwa katika Mtwala wa Kireno wa wilaya ya Mueda kwamba anayo kadi ya chama cha siasa.

Askari watatu walitumwa kumkamata; na baada ya kufikishwa Bomani aliadhibiwa vikali na askari wa Kireno.

Akiwa taabani mtu alipelekwa ndani ya jela ambako alikufa baada ya muda mfupi.

Mwanamke ambaye naye ameuawa kwa njia ya mateso kama hayo ya mtu wa kwanza anaitwa Tresa Munda, ambaye alikuwa na umri wa miaka 22.